**TAARIFA YA ZIARA YA MKUU WA MKOA WA SONGWE WILAYANI ILEJE**

Kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 18-19, Septemba 2018 Wilaya ya Ileje ilikuwa imetembelewa na Mkuu wa Mkoa wa Songwe Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangela akikagua baadhi ya miradi,kuzungumza na wananchi kwenye mikutano ya hadhara pamoja na kuendelea kulitambua eneo lake la kiutawala.

Mara baada ya kuwasili kwenye Ofisi za mkuu wa Wilaya Mkuu wa Mkoa alielekea Ukumbi wa Sekondari ya Itumba ambako aliweza kuzungumza na watumishi waliopo Ofisi ya DC na Halmashauri akiwaeleza lengo la ziara yake na kuwataka kuwa mfano katika jamii .

**Mradi wa Maji wa Ilanga-Ikumbilo na Mkutano wa hadhara Kijiji cha Ikumbilo**



Mkazi wa Kijiji cha Ikumbilo-Ileje akitoa kero kuhusu mikopo kwa wanawake

Aliweza kutembelea chanzo cha maji na kujionea jinsi mifugo wanachungwa eneo hilo akiagiza viongozi wa Wilaya za Ileje na Mbozi kukaa pamoja ili kukomesha hali hiyo kwa kuwa chanzo hicho kipo mpakani na kuugiza pia baadhi ya miundombinu kurekebishwa kutokana na dosari alizoziona zikiashiria dalili mbaya kwa mradi.

Kwenye mkutano wa hadhara katika kijiji cha Ikumbilo wananchi walimweleza kukosekana kwa soko la mahindi kulivyowaathiri kimaisha kutokana na Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuhitaji kiasi kidogo cha mahindi ikilinganishwa na mavuno yalivyo makubwa pamoja na mikopo kwa wanawake Mkurugenzi akiahidi kufuatilia.

Mhe. Mkuu wa Mkoa na watalaam wake waliwaeleza wananchi kuondokana na kuuza mahindi badala yake waanzishe viwanda vitakavyotoa unga na kutengeneza vyakula vya mifugo na akiahidi kusimamia taratibu za usambazaji wa mbolea ya kupamndia ya ruzuku.

**Mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Isongole**



**Diwani wa Kata ya Isongole-Ileje Mhe.Gwalusako Kapesa akitoa kero za Kijiji cha Isongole kwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe.**

Wananchi wakiongozwa na diwani wao Mhe.Gwalusako Kapesa waliweza kuwasilisha kero mbalimbali zikiwemo shida ya maji hasa kusuasua kwa Mradi wa Maji wa Itumba-Isongole,kuwekwa kwa kifusi kisichofaa katika stendi ya magari na kukosekana kwa soko la mahindi.

Majibu ya kero hizo yaliweza kutolewa,Mkuu wa Mkoa akitoa maagizo kwa viongozi wa wilaya kuhakikisha yaweze kufanyiwa kazi kwa tarehe alizozitoa.

Kuhusu kero ya maji,aliahidi kwenda siku iliyofuata kuliona tanki lililolalamikiwa kuwa lina nyufa,pamoja na kuiona stendi baada ya kushindwa kwenda muda huo kwasababu ya giza.

**Kutembelea stendi na tanki la maji linalojengwa Isongole**



Brigedia Nicodemas Mwangela RC wa Songwe(aliyevaa kijeshi) akishuka kwenye ngazi baada ya ukaguzi wa tanki la maji linalojengwa Isongole-Ileje

Ikiwa ni siku ya pili ya ziara yake Brigedia Jenerali Mwangela aliweza kutembelea standi na kujionea kifusi kilichowekwa akiahidiwa na uongozi wa wilaya kulifanyia kazi kutokana na kukosekana kwa miundombinu pia ya kukabiri maji ya mvua.

Baada ya uchunguzi kwenye tanki,akishirikishwa pia mwananchi aliyetoa kero hiyo, ilibainika kuwa hakukuwa na ukweli wa uwepo wa nyufa mhusika akikiri kukosa elimu ya ujenzi hata hivyo,alipongezwa kwa kuwa mfuatiliaji wa mradi huo.

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Ibaba**



**Jengo la Mama na Mtoto linaloendelea kujengwa katika Kituo cha Afya cha Ibaba-Ileje**

Aliweza kujionea ujenzi ulivyokwenda akipongeza ubora wa majengo lakini akawataka watalaam wa ujenzi toka halmashauri kusimamia miradi hiyo baada ya kuona kuna makosa katika kuchimba mashimo ya vyoo akisema kazi inaporudiwa huwa kero.

**Kutembelea migodi ya Makaa ya Mawe ya Kiwila na Kabulo**



Sehemu ya makaa ya mawe katika Mgodi wa Kabulo-Ileje

Baada ya safari ndefu ya milima na mabonde kiongozi huyo aliweza kufika kwenye mgodi wa Kaburo uliopo kwenye Mlima Kabulo porini kunakohitaji barabara nzuri ili kusafirisha maliasili hiyo inayochimbwa juu ya ardhi kama kifusi cha barabarani.

Pia aliweza kutembelea mgodi wa Kiwila-Ileje ambao ni mgodi wa kwenda chini ya ardhi(under mining) ni mgodi uliokuwa ukivuma sana miaka 20 iliyopita,badaye ulizua mjadala mzito bungeni kutokana na ubinafsishaji wake ulivyokuwa umefanyika

Mgodi huu kwa sasa upo chini ya serikali kupitia Shirika la Madini (STAMICO) zikiwa juhudi kubwa za wazalendo kuupigania kutokana na ulivyokuwa umebinafishwa.

binafsi

## 6. Mkutano wa hadhara kijiji cha Kapeta na majumuisho ya ziara

Wananchi waliweza kufahamiana na kiongozi huyo na kutoa kero zao zikiwemo za kukosekana kwa soko la uhakika zao la kokoa,kusimama kwa uzalishaji mgodi wa Kiwila jinsi ulivyowaathiri kimaisha na kero ya kukosekana kwa barabara ya mkato ili kufika Makao Makuu ya Wilaya ya Ileje.



Zao la kokoa ambalo kwa sasa halina soko kwa wakulima wa Kapeta-Ileje

Madai ya wananchi kwa uongozi wa mgodi wa Kiwila yalikubaliwa ili kusikilizwa kwenye eneo la mgodi ambapo walinzi waliobakizwa kazini walimwomba kiongozi huyo kuwasaidia akijitokeza mama mmoja aliyedai mme wake alipata ulemavu lakini hadi sasa hajalipwa kitu.

**Mkuu wa Mkoa anataka nini kwa Wanasongwe?**

Anataka wakazi wote wa mkoa huu kushikamana kwa kuunganisha mawazo yetu,nguvu zetu taaluma zetu na vipaji vyetu kwa kutumia rasilimali tulizonazo katika kujiletea maendeleo.

Anataka mawasiliano ya kimaendeleo yaimarishwe ili kuufanya mkoa huu kuwa kijiji kidijitali,pia tukitoa taarifa za watu wenye mipango mibaya dhidi ya mkoa wetu wakitufanya tusomeke vibaya kitaifa na kimataifa kwa mambo ya aibu.

Anataka viongozi wa umma kujenga tabia ya kusikiliza wananchi kwa kuwa kiongozi mzuri ni yule anayesikiliza shida za watu na kuzifanyia kazi.

Anataka jamii nzima ya Songwe ijue matumizi sahihi ya vyakula ili kuepuka na udumavu wa akili na miili.

**Anachukia nini?**

Hataki taarifa au takwimu za uongo kwani zina gharama kubwa hupoteza muda na rasilimali pasipo sababu,kama yule aliyesema tanki la Isongole lina nyufa bila kuwa na uhakika kabla ya kuzitoa.

Pia hapendi imani za kishirikina kama hawa **"rambarambi**" wenye kuwasha moto wa uchonganishi katika familia na jamii ambao kuuzima au kuirejesha jamii katika mahusiano ya awali huchukua muda mrefu au kushindkana.

Anachukia vyoo vibovu ambavyo vinajengwa bila kufuata ramani za ujenzi wa vyoo bora ambazo zipo kila kijiji hadi tarehe 13/09/2018 kila mmoja awe na cho bora vinginevyo sheria itachukua mkondo wake



**Moja ya vyoo vinavyopigwa vita na viongozi wa Wilaya ya Ileje kupitia kampeni ya Jenga choo na Mkude (hiki kilipigwa picha Kijiji cha Itale)**

## Wanasemaje viongozi wa Wilaya hiyo?

Viongozi wa Wilaya hiyo kwa ujumla wao walimwomba kiongozi huyu kukaza buti katika kuhakikisha kuwa makaa yam awe yanakuwa moja ya njia za kuunyanyua mkoa huo ulio na umri wa miaka miwili hivi tangu kuanzishwa kwake.

Mkuu wa Wilaya Ndg.Joseph Mkude alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa tayari kwenye mwaka wa fedha huu serikali imetenga bilioni 8 kwaajili ya mgodi wa Kiwila ili uanze kurudi mahali pake kiuzalishaji.

Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Ubatizo Songa ameendelea kutaarifu umma kuwa mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwila upo Ileje mkoa wa Songwe na si vinginevyo.

Tabia ya uzalendo kwa Taifa Letu iwe wimbo wa kila mmoja kimatendo pamoja na kujiepusha kuwa chanzo cha kero kwa wengine bali uwe kimbilio na mtatuzi wa migogoro.

## Maoni yangu je?

Nakubaliana na wahenga kuwa;Taaluma zote duniani iwe sheria,ualimu,habari,kilimo,uchungaji wa kanisa,udaktari,ulinzi na usalama na mengine yote yanayofanana na hayo ni kumfanya binadamu aishi kwa amani hapa duniani,Tanzania Songwe,Ileje mtaani na nyumbani kwake akifurahia maisha yake.


Imeandaliwa na:

Daniel J.Mwambene

Kitengo cha Habari Halmashauri ya (W) Ileje

www.ilejedc.go.tz